

## NAMBA 6: MARKO 8:27–38. YESU NI NANI? MAISHA YA MFUASI WA KWELI

Niwaombe turejee katika injili ya Marko, nasi tusomea **sura ya nane, mstari wa ishirini na saba hadi thelathini na nane**. Hii ni sehemu ya katikati katika injili. Na pia ni kifungu muhimu sana katika injili. Utaona katika notisi zako kwamba, kuna vichwa viwili vya habari katika kipindi hiki. "*Yesu ni nani? na "maisha ya mfuasi wa kweli"*". Katika sehemu hii ya kwanza, tutaangalia swali hili, Yesu ni nani? Katika sehemu ya pili, tutaangalia kile kinacho-maanishwa kuwa mfuasi wa kweli wa Yesu. Hebu tusome **mistari ya ishirini na saba hadi thelathini na nane**. "*Kama mtu yeyote akitaka kunifuata, lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, na kunifuata*". Hii ni mistari ambayo tunajua vyema, lakini namna kuitumia katika maisha yetu ndiyo changamoto kubwa. Kwanini? Kwa sababu, kama binadamu, sisi tu wabinafsi na hatutaki kujikana wenyewe. Na hatupendi matatizo katika maisha yetu. Tungependa kuwa na maisha rahisi, lakini mara nyingi, kama wewe ni Mkristo, maisha yanaweza kuwa magumu, kwa sababu ya wewe kumfuata Kristo.

Kwanza, Yesu ni nani? Hili ndilo swali ambalo wanafunzi wanaulizwa. Na hili pia ni swali muhimu zaidi duniani. Katika hatua hii katika injili ya Marko, Yesu anatembelea kaskazini mwa **Israeli**. Anatembelea mahali panapoitwa **Kaisaria Filipi** - ambayo iko takribani kilometa **hamsini** kaskazini mwa **Galilaya**, mbali mbali kutoka miji na majiji makubwa. Tunaweza kusema kwamba Kaisaria Filipi ulikuwa porini! Pia ni moja ya sehemu nzuri sana za Israeli. Kuna miti na mito nyingi, na milima pia. Na mlima mkubwa katika Israeli upo hapa – unaitwa mlima **Hermoni**. Na kutoka katika mlima huu mkubwa, unatoka mto **Yordani**, na maji ambayo hutoka kwenye mlima huo ni masafi sana – na pia baridi sana! Na sababu yake ni kwamba juu ya mlima Hermoni, wakati mwingine kuna theluji nyingi, na hivyo maji yake yako baridi sana. Hata sasa katika Kaisaria Filipi bado unaweza kuona magofu ya majengo ambayo yalijengwa na **Herode**. Unaweza pia kuona magofu ya mahekalu madogo madogo, mahali ambapo watu walienda kuabudu miungu ya kigeni. Ni eneo linalo-husiana na dini za kipagani na ibada ya sanamu. Ni hapa Kaisaria Filipi ambapo Yesu alitambuliwa na wanafunzi wake kama Masihi wa kweli wa dunia.

Na walivyokuwa wakitembea kuelekea Kaisaria Filipi, Yesu anawaambia wanafunzi wake katika **mstari wa ishirini na saba**: "*watu wanasema mimi ni nani?*"? Na utaona katika **mstari wa ishirini na nane** kwamba walimpa majibu **tatu**: baadhi ya watu wanasema kwamba, '*wewe ni Yohana Mbatizaji*'. Watu wengine wanasema kuwa '*wewe ni Eliya*', na baadhi ya watu wanasema '*wewe ni mmoja wa manabii*'. Kwa wakati huu, Yesu alikuwa akifanya huduma yake kwa takribani miaka miwili. Alikuwa ameshakuwa mtu maarufu.

Watu walimjua yeye ni nani, kwa sababu ya mafundisho yake, na miujiza yake. Watu waliweza kusafiri kwa kilometa nyingi ili kwenda kumsikiliza akihubiri. Watu wengi walifikiria kuwa alikuwa ni mtu mwema, mwalimu mwenye nguvu, na mtu aliyefundisha kwa mamlaka. Lakini hawakujua kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu. Watu wengi hawakufikiria kuwa alikuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa.

"*Watu wanasema mimi ni nani*", Yesu aliuliza. Na leo, swali hilo hilo linaulizwa, na linajibiwa na mamiloni ya watu duniani kote kwa majibu yaleyale. Ukiuliza swali hilo hilo kwa Muislamu, wangeweza kusema, Yesu ni nabii wetu. Watu wengine wanaweza kuamini kwamba Yesu aliishi duniani miaka **elfu mbili** iliyopita. Watu wengine wanaweza kuamini kuwa alikuwa mtu mzuri, na mwalimu mwema – lakini hiyo ni yote. Hawanafikiri yeye ni Mwana wa Mungu. Watu wengi katika nchi za Magharibi, hawajali Yesu alikuwa ni nani. Hata kama alikuwa mwalimu mzuri ambaye aliwaponya wagonjwa, wao hawafikirii kuwa ni jambo lenye umuhimu leo.

Kuna maoni na mawazo mengi kuhusu Yesu kuwa alikuwa ni nani - lakini kwa kusikitisha, watu wengi hawaamini kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu. Lakini utaona katika **mstari wa ishirini na tisa** kuwa Yesu anawauliza wanafunzi wake swali lile lile. *"Vipi kuhusu ninyi, mnasema mimi ni nani?"* Na Petro alijibu kwa haraka. Yeye anaeleza kwa uwazi kabisa: *"Wewe ni Kristo"*. Na maneno hayo manne ni muhimu sana kwa injili. Petro anasema hapa: *"Yesu ndiye Masihi"*. Neno *'Kristo'* ni neno la Kiyunani, na neno *'Masihi'* ni neno la Kiebrania, lakini yanamaanisha kitu kimoja. Kristo na Masihi maana yake; *'mpakwa mafuta'*.

Kwa Wayahudi, maneno haya yalikuwa ni ya muhimu sana. Petro anasema wazi kuwa Yesu ni Masihi – mtu ambaye Israeli imekuwa inamsubiri, tangu wakati wa mfalme **Daudi**, ambaye aliishi miaka **elfu moja** kabla ya Yesu. Petro anasema waziwazi - Yesu ni Masihi ambaye aliahidiwa katika Agano la Kale, na kwamba hii ilikuwa ni habari kubwa sana! Ninafikiri kwamba habari ilimfanya Yesu kuwa na furaha sana. Yesu alijua Yeye alikuwa nani, na alijua kile alichokuja kukifanya, lakini anapomsikia mmoja wa wanafunzi wake akisema maneno hayo, nafikiri iliweka tabasamu juu ya uso wake! *"Petro, umenifuata kwa miaka miwili. Umesikia mafundisho yangu, na umeiona miujiza. Ninafuraha kwamba unaamini kuwa mimi ni Masihi."*

Lakini angalia kile ambacho Yesu anakisema katika **mstari wa thelathini**. Badala ya kuwaambia wanafunzi wake waende na kueneza habari hii kwa ulimwengu, yeye anawaonya kuwa wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye ni Masihi. Kwa nini?

Kwa nini Yesu aliwakataza wanafunzi wake wasiwaambie watu kuwa yeye alikuwa ni Masihi? Hii ilikuwa ni habari kubwa. Hii ilikuwa ikiwasisimua wanafunzi – lakini Yesu anawaambia, wala msimwambie mtu yeyote. Kwa nini? Kwa sababu hakutaka kulazimisha mapambano na msugvano na viongozi wa kidini kwa wakati huu. Hakutaka umati huo kupata msisimko juu ya hili. Watu walikuwa wamesubiria ujio wa Masihi kwa miaka elfu, na kama wangelitambua kuwa Yesu alikuwa ni Masihi, wangeweza kujaribu kumlazimisha kuwa mfalme wao. Walikuwa wanasubiri Masihi - lakini Yesu alijua kwamba atakuwa tofauti sana na Masihi waliokuwa wakimtarajia. Watu wa Kiyahudi, na wanafunzi, walifikiri Masihi atakuja na kuiondoa jeshi la Kirumi. Walifikiri Masihi atakuja na kupigana dhidi ya Warumi – lakini Yesu hakuja kufanya hayo. Naye alikuwa ameshawaambia wanafunzi wake waziwazi kile alichokuwa amekuja kukifanya.

Angalia **mistari ya thelathini na moja na thelathini na mbili**. Kisha akaanza kuwafunza kwamba angeteseka, na kukataliwa na viongozi wa dini – na ya kwamba wangelimuua. Pia aliwaambia kuwa, baada ya siku tatu, atafufuka tena kutoka kwa wafu. Je, waweza kufikiria jinsi ambavyo wanafunzi walivyojisikia? Walikuwa na furaha kwamba Yesu alikuwa Masihi - lakini baadaye Yesu ana-waambia kwamba angeuawa. Suala hili kwao, halikuwa na maana kwao. Walitazamana wao kwa wao, na hawakuweza kuamini kile walichokisikia. Masihi aliyeahidiwa hawezi kufa! Hakuna uwezekano wa jambo hili kutokea. Je, mfalme kama huyo anawezaje kuteseka na kufa? **Petro** hawezi kuamini kile ambacho Yesu anakisema. Angalia kinachofanyika katika **mstari wa thelathini na mbili**. *"Petro alimpeleka Yesu kando, na akaanza kukemea"*. Mtu yule ambaye alikuwa amekwisha kutangaza kuwa Yesu ni Masihi, kwa sasa anampeleka Masihi pembeni, na kumkemea. Hebu fikiria Petro akiuweka mkono wake kuizunguka shingo ya Yesu, na kumwambia: *"hicho si kile kitakachotokea kwa Masihi. Wewe ndiye uliyeahidiwa; wewe ndiye yule ambaye utatuokoa kutoka kwa Warumi; wewe ni Mwokozi; kwa hiyo acha kuanza kuzungumzia juu ya wewe kuuawa."*

Huyu hapa Petro akimkemea Mwana wa Mungu! Na wakati mwingine, sisi nasi tuko sawa na Petro. Nina uhakika kuwa kumekuwa na nyakati ambazo tumemkemea, au kumhoji Mungu. Labda, kwa wakati uliopita umewahi kumwambia, mimi sikukubaliana na jinsi unayofanya mambo hapa.

Baba Mungu, kwa nini unaruhusu hili litokee? Tuliomba kuhusu hili, lakini wewe haukusikiliza! Tuliomba kwamba mtu huyu angeponywa, lakini haikuwa hivyo. Ingekuwa bora kama ungefanya hili, na sio hilo. Tunajaribu kubishana na Mungu wakati mwingine.

Wakati mwingine hata tumemkemea kwa kutokufanya kile tulichotaka yeye akifanye. Sisi tuko kama Petro. Sisi tumeshindwa kuona kwamba Mungu ni mtawala wa dunia, na ya kwamba mara nyingi, Yeye ana mpango tofauti na wa kwetu. Twaweza tusiuelewe mpango wake, kama vile Petro ambavyo hakuuelewa mpango wa Yesu wa kusulubiwa, lakini hatupaswi kumkemea.

Katika **mstari wa thelathini na mbili** Yesu anawataka wanafunzi wake wajue kwamba atauliwa. Je, mstari unasema nini? "*Alizungumza waziwazi kuhusu hili*". Alikuwa hatumii mifano. Alikuwa hasimulii hadithi. Aliwataka waelewe kuwa angeliuawa. Hakuwa akificha chochote hapa. Kwa kweli, moja ya madhumuni ya Marko katika kuandika injili yake, ilikuwa ni kuonyesha kwamba kifo cha Yesu haikuwa ajali - lakini ulikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu wa wokovu. **Mara tatu** katika sura **tatu** tofauti, Yesu anawaambia wanafunzi wake kile kitakachotokea kwake. Anawataka wajue. Na Marko anataka ulimwengu ujue kuwa kifo cha Yesu haikuwa ajali. Anataka ulimwengu ujue kuwa Yesu alikuja duniani ili kufa. Na Yesu anawaambia wanafunzi wake: "*kwa kweli Mimi ndimi Masihi, lakini si aina ya Masihi mnayemfikiria ninyi. Mimi pia ni mtumishi wa mateso, na ambaye pia nitauliwa. Na Petro, nataka ujue kwamba, hakuna kitu kitachozuia jambo hili lisitokee. Nimekuja kufanya mapenzi ya Baba yangu*".

Kwa kweli, Yesu anaongea na Petro kwa uthabiti sana hapa, katika **mstari wa tatu**. Angalia kile kinachosemwa. Kwa kawaida Yesu ni mvumilivu na mpole sana kwa wanafunzi wake, lakini hapa, Yeye anainua sauti yake na anamkemea Petro. "*Nenda nyuma yangu Shetani. Hauyajui mambo ya Mungu, ila tu mambo ya wanadamu*". Aisee! Yesu ana hasira hapa. Inaonekana kana kwamba Yesu anamwita Petro, Shetani! Kwa nini Yesu afanye hivyo? Je, ni kweli yeye ana haja ya kumkasirikia Petro? Je, yeye ana haja ya kumwita Shetani? Kumbuka hili, Yesu alikuwa amekuja duniani kwa sababu moja – na hiyo sababu ilikuwa ni kufa msalabani. Na huduma yake yote, Yesu angejaribiwa ili kuuacha mpango huo.

Hebu kumbuka kile kilichotokea jangwani, mara tu baada ya ubatizo wake. Shetani alimjaribu Yesu kufanya mambo **matatu**. Kubadilisha mawe kuwa mkate. Kuruka kutoka hekaluni. Na kusujudu, na kumwabudu. Na kama Yesu angeinama chini na kumwabudu Shetani, ingemaanisha kwamba yeye hakuwa na haja tena ya kwenda msalaba. Angeweza kuyaepuka maumivu na mateso. Kumbuka, Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, lakini pia alikuwa mwanadamu, kama sisi. Japokuwa alijua kwa hakika kuwa alikuwa amekuja kufa msalabani, kulikuwa na nyakati katika huduma yake, ambapo hakutaka kufanya hivyo. Angejaribiwa kuukana msalaba kwa kusema 'hapana.'

Wakati wa majaribu **matatu**, Yesu anamwambia Shetani haswa kile anachokisema kwa Petro: "*nenda mbali nami Shetani*". Yesu anaisikia sauti ya Shetani ndani ya Petro – na lazima awe imara sana pamoja naye. "*Petro, usinjaribu kusema 'hapana' kwa msalaba. Unaweza ukajaribu kunizuia nisiende msalabani, lakini wewe haujui nini nilichokuja kukifanya*". Kwa njia moja, anazungumza na Petro, na kwa njia nyingine, Yesu anazungumza na Shetani. "*Toka katika njia yangu Shetani. Unaweza kujaribu kunizuia. Wanafunzi wangu wanaweza hata wakajaribu kunishawishi mimi nisiende msalaba - lakini unahitaji kujua, mimi naenda msalabani ili kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Nenda nyuma yangu Shetani*". Ingawa wanafunzi walitambua kwamba Yesu alikuwa ni Masihi, bado hawakuelewa kile alichokuwa amekuja kukifanya. Yesu ni nani? Yeye ni Masihi. Na kama tutamfuata Yesu, tunatakiwa kuishi kama vile Yesu alivyofanya. Na hii inatuleta kwenye hatua yetu ya pili.

Kama tutakiri kuwa Yesu ndiye Kristo, kama vile Petro alivyofanya, basi tunapaswa kumtii na kufuata amri zake. Tunapaswa kumwanguka Yesu ambaye ni mfano wetu. Na hapa ndipo mafundisho haya yanapokuwa changamoto kwetu. Tunaweza kuwa na furaha kusimama kanisani, na kusema kwamba tunaamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu; Yeye ni Masihi, lakini Je, tunafurahia kufuata mfano wake katika maisha yetu? Angalia kile ambacho Yesu anatuambia tukifanye. **Mstari wa thelathini na nne** ni muhimu. Anatumia sisi tayasikie maneno haya. *"Kama mtu yeyote akitaka kunifuata, lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake na anifuata"*. Haya maelezo yana maana halisi ya kuwa mfuasi wa kweli wa Kristo. Tunaujua mstari huu vizuri sana, lakini, je, ni kweli tunajua maana yake ni nini?

Wakati mwingine kile kinachotoka katika midomo yetu, kinaweza kuwa kimejaa kujitoa kikamilifu sana kwa Kristo - lakini matendo yetu na tabia zetu, hazionyeshi kama tumedhamiria kumfuata Kristo. Jikane mwenyewe, chukua msalaba wako, na kumfuata Kristo, inamaanisha kwamba Yesu ni kipaumbele cha **moja** - na unajitolea kufanya kile anachokuambia kukifanya, hata kama wewe hutaki kufanya hivyo. Kama sisi ni wafuasi wa kweli wa Kristo, tutamtii na kumweka wa kwanza katika kila eneo la maisha yetu. Anatuomba kwamba tuzifishe nafsi za kujitegemea, na kumweka Yesu kuwa wa kwanza. Anatumia tuseme: Bwana, si mapenzi yangu, bali ya kwako! Anatuomba tupite katika njia yake, na si katika njia yetu wenyewe. Anatusihi tukatae dhambi kwa kuiambia dhambi 'hapana'. Anatuomba tujisalimishe kikamilifu.

Kumbuka, tumenunuliwa na Yesu kwa bei kubwa. Sisi tu mali yake. Sisi ni watumishi wake. Sisi ni watoto wake. Na hivyo hii ina maana kwamba tunapaswa kuyasalimisha maisha yetu kwake, katika mambo yote tunayoyafanya. Na hii ni changamoto kwetu, kwa sababu wakati mwingine, tunataka kujipendeza wenyewe, na sio Mungu. Tunataka kwenda njia yetu wenyewe, na si yake. Lakini Yesu anasema, kama mtu yeyote angenifuata mimi, basi lazima ajikane mwenyewe, na kuuchukua msalaba wake. Hiyo inamaanisha nini? *"Chukua msalaba wako"*. Naam, tunajua kwamba Yesu alichukua msalaba wake, na kuupeleka sehemu ya njia kuelekea Golgotha. Je, unafikiri kwamba Yesu alitataka sisi twende msalabani? Unafikiri alitaka tuyaipate maumivu ya kupigwa misumari msalabani. Hapana - bali alikuwa tayari kuuchukua msalaba wake, na kufa kwa ajili yako na mimi. Alikuwa radhi kusema 'hapana' kwa kile alichokitaka, na kusema 'ndiyo' kwa kile Baba yake alikitaka.

Inamaanisha nini kuubeba msalaba wako? Ina maana kwamba utafuata nyayo za Kristo, hata kama maisha yatakuwa magumu. Wakati mwingine maisha ni magumu kwa sababu tunamtii Kristo. Kama wachungaji na wainjilisti tunaweza kupata dhiki kwa sababu tu sisi tunamfuata Kristo. Kama usiingekuwa Mkristo, huenda maisha yangukuwa ni rahisi. Kama ukiacha kuwa mchungaji, labda maisha yangukuwa rahisi. Misalaba unayoibeba ni matatizo unayokumbana nayo katika maisha, kwa sababu ya imani yako ya Kikristo. Yesu anasema: Jikane mwenyewe, chukua msalaba wako, na ufuate mfano wangu. Angalia katika **mstari wa thelathini na tano**: *"Yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yeyote atakayepoteza maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, atayaokoa"*. Ni njia rahisi kwamba tunapaswa kumruhusu Kristo kuwa mtawala wa maisha yetu. Kama unaishi maisha yako mwenyewe, hatimaye utayapoteza – lakini kama unaishi maisha yako kwa ajili ya Kristo, utayaokoa.

Sikuzote nashangaa ninaposoma habari za baadhi ya wamisionari wa zamani, ambao walisafiri kwenda nchi za mbali, ili kuihubiri injili. Siku hizo hapakuwa na ndege au magari. Ulila-zimika kusafiri kwa mashua, au kutembea kwa miguu ili kufika mahali unapohitaji kufika. Ilikuwa ni kazi ngumu kwenda maeneo haya. Wamisionari hawa waliuia nafsi zao na waliukubali ugumu huo kwa ajili ya Kristo. Baadhi yao walikwenda kwenye maeneo, ambayo injili haijawahi kusikika huko tangu

awali. Baadhi yao walikwenda katika maeneo ambayo watu wake waliichukia injili. Baadhi ya wamisionari hawa hata walienda mahali ambapo wamisionari wengine walikuwa wameuawa. Baadhi ya wamisionari hata waliweka mali zao kwenye jeneza, na kwenda pamoja nalo, kwa sababu hawaku-fikiria kuwa wangerejea nyumbani.

Miaka mia mbili iliyopita, mmisionari kutoka Uingereza aliyetitwa **James Calvert**, alikwenda **Visiwa vya Fiji**, karibu na Australia. Watu walioishi huko walikuwa hawajaisikia injili. Walikuwa na dini yao wenyewe, na walikuwa '*wala watu*' – waliwaua, na kula wanadamu. Ilimchukua James miezi mingi kufikia katika Visiwa kwa mashua - na walipokuwa wakisafiri, nahodha wa mashua alijaribu kumshawishi James asiende katika visiwa hivyo. Alimwambia: "*Usiende katika visiwa, kwa sababu kama utaenda, hakika utapoteza maisha yako. Usiende*". Sikiliza jibu la **James Calvert**: "*Kwa kweli, sisi tulishakufa kabla ya kuja hapa*". Kwa maneno mengine, katika kuamua kumtii Kristo na kuja hapa, ni tayari tumeshaua tamaa zetu wenyewe. Sisi tumeshayatoa maisha yetu, na kuzi-ua nafsi za umimi. Tunawezaje kuishi maisha yetu kama hivi? Ni pale tu tunapojitoa kikamilifu kwa Kristo, na kumpa maisha yetu, na kumruhusu yeye atuongoze; ni pale tu hamu yetu juu ya Yesu ina nguvu sana kuliko hamu yetu ya kitu kingine chochote.

Na kisha hatimaye katika kifungu hiki, utaona kwamba sura inaishia kwa maneno mengine yenye changamoto sana. **Mistari ya thelathini na sita hadi thelathini na nane.** "*Itamfaidia nini kama mtu akiupata ulimwengu wote, lakini akaipoteza nafsi yake? Au ni kitu gani mtu anaweza kutoa badala ya nafsi yake? Kama mtu yeyote atanionea aibu mimi na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinifu na cha dhambi, Mwana wa Mtu naye atamwonea aibu atakapofika katika utukufu wa Baba yake*". Kila mara ninapouangalia mstari huo, ninakumbushwa kazi yangu ya kwanza. Wakati nilipomaliza shule. nikiwa na umri wa miaka **kumi na nane**, nilifanya kazi katika bustani za nyumba kubwa sana. Kwa kweli, ilikuwa moja ya nyumba kubwa katika Uingereza! Mmiliki wa nyumba (bosi wangu) alikuwa rafiki wa Malkia, na alikuwa tajiri sana. Lakini alikufa akiwa na umri wa miaka **themanini na nne**. Na hivi ndivyo gazeti lilivyosema kumhusu huyu aliyekufa.

"*Andrew Devonshire alikuwa ni mmoja miongoni mwa watu tajiri nchini Uingereza. Katika miaka ishirini ya mwisho ya maisha yake, alijifanyia dola za kimarekani milioni arobaini kutokana na kuuza uchoraji. Nyumba yake ilikuwa na vyumba mia moja na sabini na tano! Alikuwa na watumishi wa kumpikia; watumishi wa kumfanyia usafi; watumishi wa kumwendesha na kumzungusha. Bustani ilikuwa na ukubwa wa ekari mia moja na tano, lakini eneo kuzunguka nyumba yake lilikuwa ni ekari elfu thelathini na sita! Yeye alimiliki mali huko Scotland, Ireland, na London*". Kwa maneno mengine, twaweza kusema alikuwa na kila kitu ambacho angekitaka. Alikuwa na mali. Alikuwa na pesa nyingi. Alikuwa na mashamba mengi. Alikuwa na magari mengi. **Lakini**, hiki ndicho gazeti lilikisema: "*Andrew Devonshire hakuwa mtu wa dini. Alishawahi kusema hivi: "Sivezi kuamini kuwa kuna maisha baada ya kifo. Mimi siwezi kuamini kuwa kuna mbinguni – ingawa kama kuna jehanamu, mimi kwa hakika nitaenda huko*". Ni huzuni kiasi gani hii.

**Mstari wa thelathini na sita:** "*kuna uzuri gani kwa mtu akiupata ulimwengu mzima, na bado akaipoteza nafsi yake*"? Kwa nini upate mamilioni ya dola, wakati hauijali nafsi yako? Mwili huu utaoza baada ya kufa, lakini kitu kimoja ambacho ni cha muhimu, ni roho, ambayo inaishi milele. Lakini watu walichagua kutojitoa kwa ajili ya roho baada ya kifo - badala yake wanatumia maisha yao kutafuta pesa katika maisha haya, bila kufikiria kuhusu roho zao. Andrew Devonshire alikuwa ni tajiri sana, lakini fedha zake zote hazikuokoa roho yake. Hakuamini katika ulimwengu mwingine. Hakuamini juu ya mbingu wala kuzimu. Aliishi kwa ajili ya maisha haya pekee, lakini hakufanya maandalizi kwa ajili ya maisha yajayo. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa mamilioni ya watu ambao hawamjui Yesu. Hawajali kile kinachotendeka wakati wanakufa. Wote wanawajali hapa duniani. Na

Yesu asema. "*ni jambo zuri kwa mtu kupata ulimwengu wote, lakini bado kuacha nafsi yake*"? Hakuna kitu ambacho mwanadamu anaweza kutoa, kwa ajili ya kubadilishana na nafsi yake. Ni nini kilicho muhimu kwako? Maisha haya au yale yajayo?

Yesu anamalizia kwa kutoa onyo kubwa sana katika **mstari wa thelathini na nane**: "*kama mtu yeyote ananionea aibu mimi na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinifu na cha dhambi, Mwana wa Mtu naye atamwonea aibu atakapofika katika utukufu wa Baba yake*". Kwa maneno mengine, usimwonee aibu Yesu. Wakati mwingine, watu wanaweza kukucheka wewe kwa kuwa mchungaji. Wanaweza wakajaribu kufanya maisha yako kuwa magumu, kwa sababu tu wewe ni Mkristo. Wanaweza wakaicheka injili. Wanaweza wakajaribu kukufanya uwe na mashaka na maneno ya Yesu. Usimwonee aibu Yesu au injili yake. Yeye ni Bwana, na ni Mwokozi wetu, naye aliyatoa maisha yake kwa ajili yako. **Paulo** anasema hivi katika **Warumi sura ya kwanza, mstari wa kumi na sita**: "*Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletayo wokovu, kwa kila aaminiye.*" Hata wakati ambapo Paulo alipokabiliana na kifo kwa sababu ya imani yake, hakuweza kuionea aibu injili. Unaposoma kuhusu wanaume na wanawake katika historia, ambao walikufa kwa ajili ya imani yao, jambo ambalo utaona ni kwamba hawakuogopa kufa, na hawakumwonea aibu Yesu.

Miaka michache iliyopita, wakati tulipokuwa tukijifunza kitabu cha barua ya kwanza ya **Petro**, nilikuambia habari kumhusu mtu mmoja aliyeitwa **Polycarp**, ambaye alikufa kwa ajili ya imani hii kwa sababu hakuwa na aibu juu ya Yesu. Acha nikwaambie tena habari hiyo, kwa sababu ni habari yenye nguvu sana. Polycarp aliishi katika mji wa **Smirna** miaka elfu mbili iliyopita. Ulikuwa ni mji katika **Asia Ndogo** – ambao kwa leo, sisi tunauita **Uturuki**. Alikuwa ni mwanafunzi wa mtume **Yohana**, na baadaye akawa askofu wa Smirna. Kama wewe ungelishi katika mji Smirna wakati huo, ungetarajiwa kumwabudu **Kaisari**, mfalme wa Kirumi. Kama usingemwabudu Kaisari ungelikuwa katika matatizo!

Moja ya maswali ambayo mamlaka ya Kirumi ingewauliza watu kila mwaka, lilikuwa hili: '*Bwana ni nani?* Na jibu ambalo ulitarajiwa kulitoa ni: '*Kaisari ni Bwana, hakuna mwingine ila Kaisari*'. Lakini, Polycarp alikataa kuyasema maneno haya. Askari wa Kirumi walitumwa kwenda kumtafuta. Wakaja mpaka mlangoni mwake, na marafiki zake waliokuwa ndani pamoja naye, wakamwomba atoroke. Lakini Polycarp, ambaye sasa alikuwa na umri wa **miaka themanini na sita**, alisema hii: '*yaacheni basi mapenzi ya Mungu yatimizwe*'.

Aliwaacha maaskari waingie mlangoni. Kisha walimkamata, na kumpeleka kwenye mamlaka ya Kirumi. Afisa alimwambia Polycarp: "*kama utamwabudu Kaisari, na kumkataa Kristo, nitakuachia huru*". Polycarp hakuwa na hofu ya tishio hili. Alisema haya: "*kwa miaka themanini na sita nitemtumikia Kristo, na Yeye hajawahi kunifanyia madhara ya kunidhuru. Nawezaje kumtukana mfalme ambaye aliniokoa*"? Kwa maneno mengine twaweza kusema, hakumwonea aibu Yesu Kristo. Hakuwa na aibu ya kuwa mfuasi wa Yesu. Kwa mara nyingine tena, afisa alimsihi amkatae Kristo: alisema "*mimi nina wanyama mwitu, na kama wewe hautaibadili akili yako, mimi nitakutupia kwao*".

Majibu ya Polycarp yalikuwa rahisi: "*Waache wanyama wa mwitu na waje*"! Hivyo afisa akamwambia tena: "*kama hautaibadili akili yako, kwa sababu wewe hauwaogope wanyama mwitu, basi nitakuuwa kwa moto*". Mara nyingine tena, Polycarp alijibu bila hofu: '*kwa nini unachelewa? Fanya unachokusudia. Mimi sina hofu. Mimi sina aibu juu ya Kristo*'. Kisha askari wakamshika, na wakaanza kumpigilia kwa misumari kwenye mbao, ili kwamba asiweze kutoroka. Lakini Polycarp aliwazuia, na akawaambia: "*Niche mimi peke yangu kama nilivyo. Mungu ambaye atanisaidia*

*kuuvumilia moto, pia atanisaidia kukaa na kubaki motoni. Hakuna haja ya kunifunga".* Kisha akaomba kwa sauti kubwa, na akajitoa mwenyewe kwa Mungu. Moto ulikuwa umeshawashwa, na alichomwa moto mpaka akafa. Hapa tunamwona mtu katika Smirna, ambaye hakumwonea aibu Yesu Kristo, hata kama ilimaanisha kifo kwa ajili yake.

Kwa hali yoyote ile ambayo unaweza kukumbana nayo katika huduma yako – simama imara, na usimwonee aibu Yesu, au injili. Na huu ndiyo ujumbe unaohitaji kuwahubiria watu wako. Msiwe na aibu na Yesu. Kwa kweli, **mstari wa thelathini na nane** ni ujumbe ambao Kanisa linahitaji kuuhubiri kwa ulimwengu. Ni onyo ambalo tunahitaji kulishirikisha pamoja na wale, ambao hawamjui Kristo. Tumeitwa kuwaonya wengine kwa kile kitaka-chotendeka ikiwa hawatamgeukia Yesu. Ujumbe uko wazi kutokana na alichokisema Yesu. Wale ambao watamwonea aibu Yesu, katika maisha haya, hawakuwa pamoja na Kristo katika maisha ya milele huko mbinguni. Ikiwa watu wanaendelea kumpuuza Yesu; kama wataendelea kuionea aibu Yesu na injili, tunaambiwa kwamba wakati Yesu atakapokuja tena, atawaonea aibu wao. Na watu hawa hawawezi kukaribishwa katika ufalme wa Mbinguni. Badala yake, watapelekwa jehnamu kwa sababu ya kumkataa kwao Yesu. Usimwonee aibu Kristo.

Je, watu wanamsema Yesu ni nani? Kuna watu wengi katika miji na vijiji vyetu, ambao hawamjui Yesu ni nani - ni kazi yetu ya kuwaonyesha. Pia nadhani kwamba kuna watu wengi katika makanisa yetu, ambao kwa kweli hawamjui Yesu ni nani. Ni kazi yetu kuwaonyesha Yesu ni nani. **Na wewe je?** Wewe unasema Yesu ni nani? Kama Yesu anajisema yeye jinsi alivyo, basi tunatakiwa kumfuata Yeye. Kwa nguvu zake, na acha tujikane wenyewe, na kama tumeitwa ili kuubeba msalaba, au magumu kwa sababu ya Yesu - hebu na tufanye kwa hiari. Tumweke Kristo wa kwanza, wengine wa pili, na sisi wenyewe wa mwisho. Na tusimwonee aibu Yesu Kristo.

-----